**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 16 Februari, 2022**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 25 Disemba, 2021.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2021/2022.

**MASWALI:**

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

153. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.

Kupitia TASAF, Serikali zimeonyesha nia safi ya kuwatoa wananchi wake kutoka kwenye dimbwi la umasikini uliokithiri. Hata hivyo, ruzuku na miradi itokanayo na mpango wa kuzinusuru kaya maskini hazijasambaa katika vijiji vyenye kaya maskini za ukweli au fukara zilizopo katika jimbo la Pandani.

(a) Je, ni kaya ngapi kwa ujumla zinakidhi vigezo vya kaya masikini katika jimbo la Pandani na ngapi zinanufaika na mpango huu kwa sasa.

(b) Je, ni kaya ngapi kwa ujumla wake zinatarajiwa kunufaika na mpango huu wakati Shehia zote 388 za Zanzibar zikishirikishwa.

(c) Je, ni miradi ipi ya jamii na yenye thamani gani iliyokusudiwa kutekelezwa katika jimbo la Pandani kwa miaka mitano ijayo.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

103. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIR (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Tunashukuru Serikali kwa kujenga jengo kubwa la Mahakama Tunguu lenye kuendana na hadhi yetu.

(a) Je, wananchi waliokuwa wakilima hapo wameshalipwa haki zao zote.

(b) Wananchi wanaodai haki zao wanasikitika kuwa malipo yao hupewa kidogo kidogo mno. Je, sababu zipi zinazopelekea kutopewa fedha zao kwa pamoja.

(c) Je, ni lini watamaliziwa fedha zao na ni nani anaehusika kulipa fedha hizo.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

22. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Pamoja na maamuzi ya Serikali kuwaondosha wafanyabiashara na wajasiriamali wadogo wadogo katika maeneo ya Darajani na Michenzani Tobo la Pili na kuwahamishia katika soko jipya Kibandamaiti, bado hali ya soko lile kibiashara hairidhishi kutokana na kuwepo kwa mnada mmoja tu wa nazi. Hali hii inapelekea soko lile kutochangamka, kukosa wateja na kuendelea kufifia kila siku licha ya Serikali kutumia fedha nyingi kwa kujenga mabanda katika soko lile.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuliimarisha soko la Kibandamaiti na kulifanya kuwa na hadhi na lenye tija kwa wajasiriamali hao.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza mabanda yale kwani wapo wafanyabiashara wengi wamekosa maeneo katika mabanda na kusababisha bidhaa zao kupanga chini hali inayowapelekea kuteseka kwa jua kali na mvua.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

71. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Wananchi wa jimbo la Tumbe katika kijiji cha Shumba Viamboni na vitongoji vyake wamekuwa na matumaini makubwa juu ya Serikali yao katika upatikanaji wa huduma za afya ikiwemo huduma ya mama na mtoto katika kujenga ustawi wa afya zao.

(a) Je, ni sababu gani za msingi ambazo mpaka leo kituo cha huduma za mama na mtoto cha Shumba Viamboni hakijatoa huduma hii.

(b) Je, kuchelewa huko kwa muda mrefu hakutaathiri utekelezaji wa Ilani ya CCM ya 2020 – 2025.

85. MHESHIMIWA SULUBU KIDONGO AMOUR (Jimbo la Mkwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Licha ya juhudi za Serikali za kuimarisha hospitali zetu za Mikoa na Wilaya, bado katika hospitali ya Gamba kuna nyumba ya kukaa madaktari ambayo kwa sasa haikaliki kutokana na kuibiwa vitu vyote kwa ajili ya matumizi ya wafanyakazi hao na hivyo kupelekea Serikali kupoteza fedha za nauli kwa ajili ya kuwalipa madaktari wanaotoa huduma kutoka mjini na kurudi.

(a) Mheshimiwa Waziri baada ya kufanya ziara hospitalini hapo, Je, ni hatua gani umechukua kutokana na wizi huo uliotokea.

(b) Je, Serikali itarejesha lini vifaa hivyo vilivyoibiwa ili nyumba ya madaktari iweze kukalika.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

13. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Katika harakati za kufufua michezo Zanzibar Serikali ya awamu ya nane imeanzisha harambee maalum ya kuchangisha fedha pamoja na kutafuta wadhamini hasa katika mchezo wa mpira wa miguu.

(a) Je, Serikali imeipa kipaumbele mchezo gani katika malengo hayo.

(b) Je, matarajio ya ukusanyaji wa fedha hizo ni kwa kipindi cha muda gani.

(c) Tangu fedha hizo kuanza kukusanywa hadi sasa, ni kiasi gani kimepatikana na nini kimeanza kufanyika kulingana na lengo husika.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

36. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Hivi sasa katika maendeleo ya nchi ya Zanzibar suala la utalii ndio sekta muhimu kwa uchumi wetu. Jimbo la Nungwi kwa mfano ndiko kwenye hoteli nyingi za kitalii na hoteli hizi zinaingiza fedha nyingi lakini hadi hivi sasa barabara zinazoingia ndani kuendea mahotelini bado ni barabara zenye mabonde ambayo yanasababisha usumbufu kwa wageni ambao hasa ndio walengwa wa utalii huo.

Je, ni lini barabara hizi zitajengwa kwa kiwango cha lami hasa ukizingatia tamko la Mhe. Rais alipokuwa mgombea urais wa Zanzibar alipofika Nungwi na kuweka ahadi mbele ya wananchi kuzijenga barabara hizi.

111. MHESHIMIWA AZZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tokea usafiri wa boda boda kurasimishwa hapa visiwani Zanzibar watu wengi wamekuwa wakipoteza maisha yao na wengine kupata ulemavu wa kudumu, kutokana na ajali zinazosababishwa na mwendo kasi wanaotembea madereva wa vyombo hivi.

(a) Je, Wizara yako imechukua hatua gani katika kuondosha kabisa ajali zinazotokana na vyombo hivi hapa visiwani.

(b) Ni adhabu gani iliyowekwa kwa madereva hawa pale wanaposababisha maafa haya.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

91. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Somo la michezo “physical science” kwa sasa linafundishwa katika baadhi ya skuli za Zanzibar na wanafunzi wanafanya vizuri katika mitihani ya Taifa.

(a) Kwa nini somo hilo halijafundishwa katika skuli zote za Zanzibar.

(b) Serikali ina mpango gani wa kuwapatia vifaa vya kufundishia walimu wa somo la “physical science”

(c) Ni jitihada gani zinazochukuliwa katika kuhakikisha viwanja kwa ajili “physical science” vinapatikana.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

140. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika kuwarahisishia wananchi shughuli za kilimo, Serikali imekuwa ikijitahidi kutoa huduma za matrekta ambapo wananchi hulimiwa mashamba yao kwa gharama stahiki. Hata hivyo, kumekuwa na upungufu na ughali wa huduma ya matrekta kwa wananchi wa jimbo la Pandani kiasi ya kutokidhi mahitaji yao kwa kiasi kikubwa.

(a) Je, Serikali ina matrekta mangapi yanayohudumia katika jimbo la Pandani ukilinganisha na mahitaji halisi ya matrekta katika msimu mkubwa wa kilimo.

(b) Je, ni upi mpango wa haraka wa Serikali wa kuongeza huduma ya matrekta kwa ajili ya wakulima wa Machengwe na maeneo mengine ndani ya jimbo la Pandani.

(c) Je, Serikali haioni kuwepo kwa ulazima wa kuwaomba na kuwashirikisha wafanyabiashara binafsi kutoa huduma ya matrekta na Serikali kubeba baadhi ya gharama ili kufidia gharama halisi za huduma hiyo.

**<u>Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:</u>**

34. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Katika skuli zetu nyingi maeneo yao yanavamiwa na wananchi kwa ajili ya ujenzi au matumizi mengine.

(a) Je, Serikali ina mpango gani ya kuyapima maeneo ya skuli ili wananchi wayajue na waache kuyavamia.

(b) Skuli nyingi hazina hatimiliki, Je, ni lini Serikali itachukua juhudi za makusudi kuzitafutia hatimiliki skuli zetu.

**<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

106. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuimarisha Kampuni yake ya Uvuvi ya "ZAFICO" ikiwa ni pamoja na kuipatia vifaa vya kisasa ikiwemo meli za uvuvi.

(a) Je, Serikali kupitia kampuni hii ilipanga kununua meli ngapi za uvuvi.

(b) Je, mpaka sasa meli ngapi tayari zimeshapatikana.

(c) Kwa kiasi gani matokeo ya awali ya Kampuni ya ZAFICO yanaonesha kuwa kampuni hiyo ina tija kwenye pato la Taifa.

## III. <u>HOJA ZA KAMATI:</u>

**<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa</u>:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**16 Februari, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>.**